# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

## SHULE YA SEKONDARI USAGARA

**Barabara ya Jamatini, S.L.P. 330 Tanga, Simu: 0784-413494, ,E-mail:usagarasecondary@gmail.com**
**Website:** www.usagarasec.sc.tz

**SIMU- MKUU WA SHULE: 0784 – 413494**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0718 – 012812 AU 0717 - 357820**

**PATRON: 0769- 958584 AU 0624 - 276499**

**Kumb. Na. USS//6/24/JNG/2024/06/….** **TAREHE :13 / 05 / 2024**

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………………………**

**S.L.P ……………, Wilaya....................................., Mkoa..............................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI USAGARA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA MKOA WA TANGA KWA MWAKA WA MASOMO 2024 / 2025.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya PCB/PCM/CBG/HKL/KEC/HKCh/KLCh na HGCh.

Shule ya Sekondari Usagara ipo umbali wa Kilometa KM 2.5 toka kituo kidogo cha mabasi ya mjini ( Ngamiani) kuelekea mashariki mwa Mji wa Tanga Usafiri wa basi kutoka stendi kubwa ya mabasi Kange Mpaka kituo kidogo cha mabasi Ngamiani nauli ni shilingi 500/= na kuelekea shule usafiri ni Tax Tshs 5,000/= Bajaji 3000/= na pikipiki 2,500/=
Muhula wa masomo unaanza **Tarehe 01/07/2024** mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule **Tarehe 01/07/2024** mwisho wa kuripoti shule ni **Tarehe 15/07/2024.**

***** Siku ya kuja shuleni uwe umevaa Track suit kama ilivyoagizwa hapa chini.**

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

**2.1, SARE YA SHULE:**

(i) Mashati mawili **(2)** meupe ya mikono mifupi na yasiyobana.

(ii) Suruali mbili **(2)** za rangi ya ugoro (**brown)** zenye marinda zisizobana. Kuepuka kuchanganya rangi kama utapenda anaweza kushonea shuleni kwa sh. **18,000/=** kila moja jumla sh. **36,000/= tu.**

(iii) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi, vya kufunga kamba (sio buti).

(iv) Soksi nyeupe pair mbili na fulana nyeupe 4 ( vest)

(v) Sweta liwe rangi ya ugoro (**brown)** la mikono mirefu, shingo ya "**V"** linapatikana Shuleni kwa sh. **16,000/=** tu kama utanunulia kama utapenda kununulia hapa shuleni.

(vi) Mkanda mweusi au ugoro usio na urembo wowote wenye buckle iliyowazi katikati na Ndala za kuogea

(vii) Raba,Sandals za ngozi zenye mikanda ya Brown siyo za kuchomeka, , bukta za blue mbili (vifaa vya michezo).

(Viii) T Shirt mbili za michezo rangi ya Kijani – plain na T shirt ya shule yenye Nembo inapatikana shuleni kwa Sh. **12,000/=**

(ix) Shuka **2** za rangi ya BLUE kama utapenda zinapatikana zote shuleni kwa sh. **16,000/=tu** (kwa zote 2).

(x) Track suit moja ya Rangi ya kijani zenye michilizi meupe na soks za michezo za kijani.

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa hapo juu.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Madaftari (counter book Q3) Zinahitajika angalau 8.

(ii) Ream za Karatasi Mbili (2) moja A4 na nyingine Ruled .

(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kulingana na mchepuo wa mwanafunzi.Vitabu vya GS na BAM ni lazima kuja navyo.

(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

(v) Scientific Calculator.

(vi) Shule ina magodoro ni vyema mwanao akagharamia kiasi cha shs 20,000/= tu kukodisha kwa miaka miwili.

(vii) Njoo na sanduku moja tu la bati lisilozidi urefu wa mita 1. Na taulo 1 cotton.

(viii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

(ix) Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mfuniko; mto na foronya zake 2 za Blue na Chanadarua nyeupe.

(x) Kila mwanafunzi aje na Kwanja.

(xi) Kwa mkondo wa PCM aje mfagio wa ndani soft na reki, PCB waje na Jembe lenye mpini na squeezer ,CBG waje Jembe lenye mpini na soft broom. HKL waje na Mopper 1 na ndoo yake. KEC waje na reki na hard broom, KLCh waje na soft broom, Hard Broom na squeezer, HGCh waje na soft broom, Hard Broom na squeezer na HLCh waje na Panga na Soft Broom.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 4,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 6,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizi ziingizwe bank kuanzia 01/07/2024 na siyo mwezi sita 2024 katika akaunti ya shule Jina Usagara sekondari acc. No 41701200074 nmb. Mwanafunzi aje na Original pay slip aliyolipia kwa jina lake mwanafunzi.**

***** Aje na nakala ya (a) cheti cha kuzaliwa, (b) Nakala ya Results slip (c) Picha 3 passport size alizopiga kwa shati jeupe na background ya Blue.**

## Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi au kuruka uzio wa shule na Bweni.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni size ya brashi na zisiwe za mitindo.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB:**

1. **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOAINISHWA MWANZONI MWA FOMU JUU.**

2. **Kila Mwanafunzi aje na BIMA yake ya Afya. Au aje na Shs 54,500/= ili asaidiwe na shule kukatiwa Bima ya Afya.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

…………………………

**A.R. BIRUMO**

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

**USAGARA SHULE YA SEKONDARI,**

**S.L.P. 330,**
**TANGA.**
***Kumb Na. USS/9/4*** **TAREHE:….. / ….. / 20……**

**JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………………………………**

**A. FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**Mimi ……………………………………………………………………………….nakubaliana na sheria na taratibu zilizoorodheshwa Katika kipengere namba 3 kinachohusu sharia na kanuni za shule na kuzifuata katika kipindi chote nitakapokuwa nasoma shuleni Usagara. Natambua pia kuwa** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio kamilifu katika kila shughuli ndani na nje ya shule na Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (**Preparation**).
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. Viatu, sweta au jaketi lisilo sare ya shule vitachukuliwa na havitarudishwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Kila mwanafunzi awe na begi la mgongoni"**School Bag**" rangi nyeusi.
(i) Shule haitoi chakula maalum (**Special diet**).
(j) Shule hii ni ya serikali na serikali haina dini : Hivyo mwanafunzi anatakiwa kutokujihusisha au kushawishi wengine kujihusisha na mambo ya Imani yanayoweza kuhatarisha **usalama** wa shule na jamii kwa ujumla. **Ibada na mambo yote ya kiimani** mtakavyoelekezwa mkija shuleni kulingana na ratiba ya shule. **Shule haina ulezi wa vikundi vya kiimani.**

**Sahihi ya Mwanafunzi………………………Tarehe….. / …. / 20……. Sahihi ya dole gumba**

**********************************************************************

**B. HATI YA MZAZI KUKUBALI MASHARTI YA SHULE**

**Mimi………………………………………..………………………… wa S. L. P. ………… wilaya ya ……………………..Mkoa………………..**

**Ni Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………nimeyasoma masharti yote ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Usagara. NINAKUBALIANA/SIKUBALIANI NAYO. Pia nitasimamia utekelezaji wa sheria za shule alizopewa. Najua pia simu, utoro na uchelewaji shuleni HAVIKUBALIKI**

**PICHA YA MZAZI/MLEZI**

**Sahihi…………………………… Sahihi ya dole gumba**

**Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………..........**

**Maelezo haya yamethibitishwa na :-** **<u>Mihuri husika igongwe</u>**

1. **Mtndaji wa Kata /Kijiji………………………Jina:………………………………………Sahihi…………………………Simu:…………………..**

2. **Mtendaji wa Kitongoji/ Mtaa………………… Jina:…………………………………Sahihi………………………Simu:…………………..**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**PART A**

**To Medical Officer,**

**.......................................................................................................................**

**MR/MISS.......................................................................................................................(Name in full)**

**Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course.The examinations should include the following categories (I-II) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of a defect. Pregnarcy (category IV) will also render a girl candidate inligible for the course.**

**I.** (a) Eye-sight

(b) Hearing

(c) Limbs

(d) Speech

(e) Venereal Diseases(s)

(f) Leprosy

(g) Epilepsy

**II.** Neurosis

**III.** Other serious disease

Signature…………………………………

****************************************************************************************************

**PART B**

## MEDICAL CERTIFICATE

**(To be completed by Government Medical Officer)**

**I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.**

**I.** (a) Eye-Sigh……………………………………

(b) Hearing………………………………………

(c) Limbs………………………………………..

(d) Speech………………………………………..

(e) Venereal Diseases…………………………..

(f) Leprosy……………………………………..

(g) Epilepsy……………………………………

**II.** Neurosis

**III.** Other serious disease

**Station……………………………………………  Signature…………………………………**

**Designation………………………………………  Date: ……../ ….. / 20…….**